

SOMO LA 4

MWONGOZO WA MWEZESHAJI

KOZI YA "JUKUMU LA KUJIZIDISHA"

Kupanda Makanisa Yenye Afya



Mtando wa Kuzidisha
Makanisa Mengi Zaidi, Makanisa Yenye Nguvu

"JUKUMU LA KUZIDISHA"

MAELEZO YA MTAALA WA KUPANDA KANISA | OMEGA – MINIM

SOMO LA 1 PANDA KANISA LENYE AFYA	KUANDAA KUSHIRIKISHA HABARI NIEMA	SOMO LA 3 KUFAHAMU MPANGA WA MUNGU	KUSHIRIKISHA HABARI NIEMA	SOMO LA 4 KUWAELEKEZA WATU KUELEKEA KWENYE IMANI	SOMO LA 5 KUWAELEKEZA WATU KUELEKEA KWENYE IMANI	SOMO LA 6 WANAFUNZI WANAOKUA
IBADA	Misingi ya Kibilia Ya Makania Yenye Afya	Misingi ya Kitheolojia Ya Makania Yenye Afya	Misingi ya Kimisolojia Ya Makania Yenye Afya	Misingi ya Kimakakati ya Makania Yenye Afya	Kuijili Injili	Ukuaji wa Mkristo: Kristo Kituo Muiimu (Kristo kama Klini)
SEHEMU YA 1	KANISA LENYE AFYA NI NINI?	RAMANI YA KIROHO: KANUNI ZA UTAFITI WAKO	MUNGU ANANIONYESHA NINI: SHIRIKISHA UTAFITI WAKO	HAKI KWA IMANI	VIZUZI VWA INJILI	WITO MKUU NA KUPANDA KANISA
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi/Usahihii	Kazi, Andiko, na Muktadha	Maono, Andiko, na Muktadha	Tambuliwa Katika Wito wa Kimungu	Unjilisti	Unjilisti, Uanafunzi
SEHEMU YA 2	NANI MPANDA KANISA LENYE AFYA	HIKI INDICO YESU ALICHONIFANYIA! KUELEZE NA KUSHIRIKISHA USHUHUDA WAKO BINAFSI	MUNGU ANANIONYESHA NINI? SHIRIKISHA USHUHUDA WAKO NA MTEMBEO WAKO WA MAOMBII	KANUNI ZA KIBIBILA ZA UONGOZI	MCHAKATO WA KUBADILKA I	KANUNI ZA KUFUASA KWENYE MAFANIKIO
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Tambuliwa katika Wito wa Kimungu	Unjilisti	Kazi, Andiko, na Muktadha	Kuaimarisha / kuwawezesha viongozi	Unjilisti	Uanafunzi
SEHEMU YA 3	KUFIKIRI – Z: MUNGU ANATAKA NINI?	KUONGOZA VIKUNDI VIDOGO	MPANGO WANGU MKUU WA KUPANDA KANISA: KUTAMBUA MAONO YA MUNGU	UNJILISTI NA KUPANDA KANISA	MCHAKATO WA KUBADILKA II	TAMBUA LENGO LAKO, TAMBUA WATU WAKO
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahihii	Unjilisti, Uanafunzi, Kuwawezesha / Kuaimarisha viongozi	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahihii	Unjilisti	Unjilisti	Unjilisti
SEHEMU YA 4	MZUNGUKO WA KUPANDA KANISA	NJIA YA II YA KUJIFUNZA BIBLIA KWA NJIA ELEKEZI: KUANGALIA NENO LA MUNGU	MPANGO WANGU MKUU WA KUPANDA KANISA: MAANA YA KAZI	KUANZISHA KIKUNDI KIDOGO	UNJILISTI WA KIKUNDI KIDOGO	NJIA YA IV YA KUJIFUNZA BIBLIA KWA NJIA ELEKEZI: KULITUMIA NENO LA MUNGU
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahihii	Unjilisti, Uanafunzi	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahihii	Unjilisti, Uanafunzi	Unjilisti	Unjilisti, Uanafunzi
SEHEMU YA 5	KWA NINI VIKUNDI VIDOGO?	NAMNA YA KUTENGENEZA MAOMBI KATIKA UPANDAJI WAKO WA KANISA	MPANGO WANGU MKUU WA KUPANDA KANISA: MAANA YA MSINGI	UNJILISTI NA KUFIKIA MAHITAI YA JAMII	UTENDAJI: UZOEFU WA KIKUNDI KIDOGO	KUELEWA MTAZAMO WA KIDUNIA
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Unjilisti, Uanafunzi	Unjilisti	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahihii	Huduma	Unjilisti	Tambuliwa katika Wito wa Kimungu
SEHEMU YA 6	NJIA YA I YA KUJIFUNZA BIBLIA KWA NJIA ELEKEZI: HEBU BIBLIA ITUFUNDISHE	TAMASHA LA MAOMBI: ZABURI 95	MPANGO WANGU MKUU WA KUPANDA KANISA: MAANA YA MIKAKATI	NJIA YA III YA KUJIFUNZA BIBLIA KWA NJIA ELEKEZI: KUTAFSIRI NENO LA MUNGU	KUWASILISHA MPANGO MIKUU	TAMASHA LA MAOMBI LA KUMSHUKURU MUNGU KWA UAMINIFU WAKE
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Unjilisti, Uanafunzi	Kuabudu	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahihii	Unjilisti, Uanafunzi	Michanganyiko wa Mawazo	Kuabudu

SOMO LA 7 TENGENEZA TIMU	SOMO LA 8 TENGENEZA TIMU	SOMO LA 9 KUWAJALI WATU	SOMO LA 10 KUANZISHA KANISA	SOMO LA 11 KUPANGA KWA AULI YA MAMBO YAJAYO	SOMO LA 12 KUENDELEA MBELE KWA UMOJA
IBADA	Kubadilishwa na Injili	Neema ni kwa wanyenyekewu	Upendo, Msingi wa Huduma	Iii Ulimwengu Upate Kuamini: Yohana 17	Kuhesabu Gharama
SEHEMU YA 1	MISINGI YA KIBILIA YA KANISA	KAZI YA TIMU: KUFANYA KAZI NA WENGE KWA USAHIIHI	UINJILISTI WA KIMAHUSIANO	KAZI ZA USHIRIKA ZA KANISA	UTANGULIZI KATIKA UWAKILI
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Mchanganiko wa Mawazo	Kuwawezesha / Kuwaimarisha viongozi	Kuwajali washirika wa kikundi kidogo	Mchanganiko wa Mawazo	Uwakili wa Rasilimali
SEHEMU YA 2	KANISA: KIUMBE HAI	KUANZISHA TIMU	USHIRIKA	HUDUMA KUPITIA KARAMA ZA KIROHO	TOBA KAMA NAMNA YA MAISHA
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Mchanganiko wa Mawazo	Kuwawezesha / Kuwaimarisha viongozi	Ushirika	Kuanganisha Mwili Kutohana na Karama za Kiroho	Uwakili wa Rasilimali
SEHEMU YA 3	KIKUNDI CHA WATU KINAKUWA KANISA LINI?	UHAI KATIKA MIADALA WA KIKUNDI KIDOGO	KUJUAL JAMII YETU	NAMNA YA KUTUMIA TATHMINI YA KARAMA ZA KIROHO	TOBA NA UREJESHO: NIDHAMU YA KANISA
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Mchanganiko wa Mawazo	Uanafunzi	Uinjili, Andiko, na Muktadha	Kuanganisha Mwili kutohana na Karama za Kiroho	Ushirika
SEHEMU YA 4	NJIA YA V YA KUJIFUNZA BIBLIA KWIA NJIA ELEKEZI; NJIA ZA KUTUMIA MAFUNZO ELEKEZI YA KUJIFUNZA BIBLIA	KUWAFUNDISHA VIONGOZI WAPYA WA VIKUNDI VIDOGO	TABIA ZA KANISA LINALOKUWA	UHAI WA VITA VYA KIROHO	MITINDO YA UONGOZI
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Uanafunzi	Uanafunzi, Kuimarisaha/ Kuwawezesha viongozi	Mchanganiko wa Mawazo	Ushirika	SEMINA YA MPANGO MKAKATI I
SEHEMU YA 5	MWONEKANO WA KIONGOZI MKRISTO	MITINDO YA KUICHANGANYA	UONGOZI WA KITUMISHI	NAMNA YA KULIONGOZA KANISA KATIKA KUABUDU	Kuwawezesha / Kuwaimarisha Viongozi
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Kuwawezesha / Kuwaimarisha viongozi	Kuwawezesha / Kuwaimarisha viongozi	Kuwawezesha / Kuwaimarisha viongozi	Kuabudu	KANISA LETU NA UKUBWA WA MWILI WA KRISTO
SEHEMU YA 6	MAHUBIRI YA KIBILIA II: KULIELEWA KUNDI / KUSANYIKO	MAHUBIRI YA KIBILIA III: KULIELEWA KUNDI / KUSANYIKO	TAMASHA LA MAOMBI: WAFFESO 3 – 5	MAHUBIRI YA KIBILIA III: KUJIELEWA WEWE MWENWEWE	Ushirika
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Kuabudu	Kuabudu	Ushirika	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahihhi	Unjiliisti

JUKUMU LA KUJIZIDISHA
Masomo ya Kupanda Makanisa Yenye Afya
Mtandao wa Huduma za Kujizidisha
Makanisa Mengi Zaidi / Makanisa Yenye Nguvu Zaidi
Hakimiliki © 2015



Masomo haya ya mafunzo ya upandaji kanisa ni mjumuisho wa kozi ya Abridged Omega na mafunzo ya Kupanda Makanisa Yenye Afya ya Mtandao wa Huduma ya Kujizidisha.

MNM imepata ruhusa kutoka katika Kituo cha Mafunzo ya Upandaji wa Makanisa na Huduma za Ulimwengu ya kuweka wazi kazi hii itumiwe na kanisa.

Unaruhusiwa na kutiwa moyo kuzalisha na kusambaza masomo haya kwa muundo wa aina yoyote yatakavyotolewa kwamba: (1) utambue chanzo (2) Onyesha ikiw marekebesho yamefanyika, (3) usitoze gharama zaidi ya ile ya kuzalisha, na (4) usizalishe nakala zaidi ya 1,000.

Kozi ya OMEGA:
Mafunzo ya Vitendo kwa Mpanda Kanisa
Hatimiliki © 2000, 2006 United World Mission.

Masomo haya mwanzoni yalimiliwi na Alliance for Saturation Church Planting na kuandaliwa na huo ubia kwa kushirikiana na Huduma ya Peter Deyneka Russian, Project 250.

Kama ungependa kuyarusha masomo haya kwenye mtandao au kama umedhamiria kutumia zaidi ya ilivyotajwa hapo juu, tafadhalu wasiliana na United World Mission, ATTN: Jay Weaver/Omega, 9401-B Southern Pine Blvd., Charlotte, NC 28273-5596, au omega_course@alliancescp.org.

Tafsiri na marekebisco/matoleo katika mazingira yako pia yanaruhusiwa.

Tunamshukuru Dr. Jerry Wofford na Dr. Jeff Hale kwa mchango wao usioweza kulipwa katika kuandaa masomo haya.

Gary Teja na John Wagenveld, wahariri wa Jukumu la Kujizidisha

www.multiplicationnetwork.org

PENDEKEZO LA MUUNDO WA SIKU 1 WA MAFUNZO YA SOMO LA 4		
	UTANGULIZI WA SOMO LA 4	2:00
	IBADA	2:15
	KUTOA TAARIFA	2:30
KIPINDI CHA KWANZA	KUHESABIWA HAKI KWA IMANI	3:00
	MAPUMZIKO	4:00
KIPINDI CHA PILI	KANUNI ZA KIBIBLIA ZA UONGOZI	4:15
KIPINDI CHA TATU	UINJILISTI NA UPANDAJI KANISA	5:15
	CHAKULA CHA MCHANNA	6:15
KIPINDI CHA NNE	KUANZISHA KUNDI DOGO	7:15
KIPINDI CHA TANO	UINJILISTI NA KUFIKIA MAHITAJI YA JAMII	8:15
	MAPUMZIKO	9:15
KIPINDI CHA SITA	KUTAFSIRI NENO LA MUNGU: KWA KUTUMIA MAFUNZO YA BIBLIA KWA NJIA YA UCHIMBUZI	9:30
	KUFUNGA	10:30
	MWISHO WA SIKU	10:45

KUSHIRIKISHA HABARI NJEMA

Somo la 4

Lengo la Kujifunza:

- Washiriki wataweza kufahamu sababu nne za kimkakati za kupanda kanisa zilizotolewa kutoka katika kitabu cha Matendo ya Mitume.
- Washiriki wataweza kutoa maana ya wazo la kitheolojia la sababu nzuri kwa maneno yao wenyewe na kujifunza namna ya kuongoza mafunzo ya Biblia na kuelezea dhana hii kwa watu wengine.
- Washiriki watalinganisha uongozi wa kidunia na wa Kikristo, wakitumia Kazi 5 za Uongozi katika Agano Jipya kwenye mzunguko wa Kupanda Kanisa, na kujadili usahihi na mwelekeo na uongozi unaofaa katika mchakato wa kupanda kanisa.
- Washiriki watajifunza na kujadili kanuni 5 za uinjilisti kwa wapanda makanisa.
- Washiriki wataendeleza mpango mzima wa mkuatano wa kundi dogo.
- Washiriki watajifunza na kuendeleza shughuli zinazofanana na aina 3 za mahusiano kati ya uinjilisti na huduma.
- Washiriki watapata na kuzitumia dhana za tafsiri za mchakato wa kujifunza Biblia kwa njia ya uchimbuzi.
- Katika Mpango Kazi wa Somo la 5, kujenga kwenye kazi iliyotangulia, kila mpanda kanisa ataongeza mpango mkuu wa kupanda kanisa. Kwa kutumia mwongozo, kila mpanda kanisa atatoa utafiti muhimu, maono, dhima, maadili ya msingi, na mkakati utakaoongoza juhudzi zake za kupanda kanisa. Kila mpanda kanisa awe na mkataba uliokubalika kutoka kwa mchungaji na kanisa linalomuunga mkono (uthibitishwe na sahihi ya mchungaji) ikiwakilisha uthibitisho wa maandishi ya mpango mkuu wa kupanda kanisa.

Utangulizi wa Somo la 4 (dakika 15)

Neno la Utangulizi la Mwezeshaji (dakika 2)

Wakaribishe washiriki kwa ukarimu, kirafiki, na kwa moyo wa dhati. Waongoze washiriki katika maombi ya pamoja kwa kifupi, iweke siku wakfu kwa utukufu wa Mungu.

Shughuli ya kuanzia: (dakika 12)

Mimi ni nani?

Andika majina ya watu wa Biblia wanaofahamika vizuri kwenye karatasi. Bandika karatasi kwenye mgongo wa kila mtu ili asiweze kuisoma. Watu wazunguke humo ndani ya chumba wakiuliza swali moja kwa wakati kwamba wao ni nani mpaka waweze kukisia majina yaliyo migongoni mwao.

Wakati wa kufunga shughuli waambie kila mmoja asimame kwenye mduara na aliambie kundi ni mtu gani wa kwenye Biblia wanamuwakilisha. Waambie kila mtu ashirikishe kitu kimoja kwa mtu wa Biblia wanachofikiri kinaweza kuwa cha muhimu kwa mpanda kanisa au katika kupanda kanisa. Kila mmoja akimaliza, waambie warudi kuketi kwenye viti vyao kwa ajili ya ibada.

IBADA MISINGI YA KIMKAKATI KWA MAKANISA YENYE AFYA (DAKIKA 15).

Muhtasari wa Maelekezo ya Mwezeshaji: Wape washiriki tofauti tofauti kazi ya vifungu vya Biblia kwa kila msingi wa kitheolojia. Waambie walisomee kundi vifungu vya Biblia kwa sauti. Liongoze kundi kuona kila kanuni ya kimisiolojia kutoka katika vifungu na wajaze sehemu zinazofanana zilizo wazi katika sehemu zao za kazi.

Uliza: “Ni nani anaweza kutuelezea maana ya “mkakati” tuliojifunza katika Somo la 3?”

Maana: MKAKATI ni kifungu cha vitendo mahsusi utakavyochukua kukamilisha MAONO na DHIMA yako wakati ukiyaishi MAADILI YA MSINGI.

Sema, “Tunaweza kufikiria mkakati kama hatua za vitendo tunazochukua kushirikisha na kuishi Habari Njema tunapopanda kanisa.”

Waelekeze washiriki kukamilisha shughuli ifuatayo katika sehemu zao za kazi.

Kuna baadhi ya misingi ya kimkakati ya kawaida ya kupanda makanisa. Hii ni baadhi:

Waambie washiriki wajaze kwenye orodha na wahakikishe na sababu zitakazotumika katika mazingira yao halisi.

- IDADI YA DATU inakuwa kwa haraka.
- Makanisa mapya yanawafikia watu wengi ZAIDI kuliko yale yaliyoimarika.
- Makanisa yaliyoimarika huelekea KUDUMAA.
- Makanisa mapya yanasaidia kuamsha makanisa YALIYOIMARIKA.
- Makanisa yanatakiwa yawe karibu na mahali WANAPOISHI waliopotea.
- Makanisa mapya YANANYUMBULIKA kwa urahisi.
- Haiwezekani kwa kanisa moja kumfikia KILA MMOJA.
- Makanisa mapya yanakuza VIONGOZI kwa haraka.
- UKARIBU unasaidia uanafunzi.

VITENDO MAHSUSI – MAONO – DHIMA - UKIYAISHI

Mpaka hapo ni misingi ipi ya kupanda kanisa ulikuwa hujawahi kuifikiria? Ni misingi ipi ambayo ingewatia hamasa watu unaofanya nao kazi ya kupanda kanisa?

Sema, "Hebu tuangalie kwa pamoja baadhi ya misingi ambayo mingine makanisa ya Agano Jipyä yalianzia."

SABABU AMBAZO KWAZO BAADHI YA MAKANISA YA AGANO JIPYA YALIANZA:

Wape kazi ya kusoma vifungu vya Biblia kwa kila msingi kwa washiriki tofauti tofauti. Waambie wasome vifungu vya Biblia kwa sauti. Elekeza kundi kuona kila msingi wa kupanda kanisa kutoka katika vifungu wasome na kujaza nafasi zilizo wazi katika sehemu zao za kazi.

Soma: Matendo 8:1-8,12

Msingi wa Kimkakati wa 1: MWITIKIO WA MATESO. Uthibitisho wa Makanisa mapya ya kwanza kupandwa nje ya Yerusalem uilitokana na mateso. Jadili namna upandaji wa kanisa unavyoweza kuwa mwitikio wa kimkakati/kiutendaji unaotokana na mateso. Waambie washiriki watoe mifano ya makanisa yaliyopandwa kama mwitikio wa mateso kutokana na uzoefu wao au ujuzi kutoka kwa wengine .

Soma: Matendo 10:1-24, 36-48

Msingi wa Kimkakati wa 2: MWITIKIO WA MAELEKEZO YA MUNGU. Mungu alitoa maelekezo sahihi kwa Kornelio na Petro. Kanisa la Kaisaria lilipandwa kwa sababu ya utii wao wa maelekezo sahihi ya Mungu. Jadili namna Mungu anavyojifunua mwenyewe kwa Kornelio na Petro. Ni namna gani walijua kwamba Mungu ndiye alikuwa akizungumza nao? Ni namna gani tunafahamu pale Mungu anapotupa maelekezo mahsus? Waulize washiriki kama wanaweza kutoa mifano ya makanisa yaliyopandwa baada ya mwitikio wa mwongozo sahihi wa Mungu ama wao wenyewe wanafahamu au wamefahamu kuitia wengine.

Msingi wa Kimkakati wa 3: MWITIKIO WA MWALIKO. Petro alikubali mwaliko wa Kornelio. Kwa sababu ya shughuli ya Mungu ambayo Petro aliishuhudia katika nyumba ya Kornelio, Petro aliweza kutambua kwamba mwaliko huu pia ulikuwa sehemu ya shughuli ya Mungu na kwa sababu hiyo Petro alibadilisha ratiba yake. Waulize washiriki kama wanaweza kutoa mifano ya makanisa ambayo yalipandwa ikiwa ni mwitikio wa mwaliko wa kuja mahali fulani ama kwa kufahamu wao wenyewe au kwa kuambiwa na wengine.

Soma: Matendo 16:9-15

Msingi wa Kimkakati wa 4: DESTURI YA UAMINIFU WA KUSHIRIKISHA HABARI NJEMA. Kanisa la Filipi lilipandwa kwa sababu Paulo alikuwa na kawaida ya uaminifu wa kushirikisha Habari Njema kila alikoenda. Paulo alikuwa njiani kuelekea Makedonia na alipitia Filipi. Kwa sababu Paulo alikuwa na desturi ya uaminifu wa kushirikisha Habari Njema, Lydia akawa Mkristo, na kanisa lilianza ambalo lingesimama kwa uaminifu na Paulo na kufanyika baraka kwa makanisa mengine. Waulize washiriki kama wanaweza kutoa mifano ya makanisa yaliyopandwa kwa sababu ya kawaida ya kushirikisha Habari Njema ama kwa uzoefu wao wenyewe au kwa ujuzi kupitia kwa wengine.

TAARIFA: (dakika 30)

Maelekezo:

- Kwa kutumia fomu ya taarifa, waelekeze washiriki washirikishe shughuli yao ya kupanda kanisa toka walipomaliza Somo la 3.
- Sherehekeza ushindi na uwatие moyo wale ambaо wanaweza kuwa wamekata tamaa. Unaweza ukahitaji kupata muda wa kuomba nao, kwa jinsi muda utakavyoruhusu, katika vikundi vidogo kuhusiana na uzoefu huu wa kupanda makanisa.
- Jibu swalı lolote kuhusu mchakato wa taarifa.

MWALIKO - DESTURI YA UAMINIFU

ABC ZA MPANDA KANISA

TAARIFA YA MWEZI

TAARIFA ZA KAWAIDA

MWEZI WA TAARIFA	USIMAMIZI WA MAHUDHURIO YA VIKAO	NDIYO	HAPANA
JINA LA MPANDAJI			
KANDA YA MPANDAJI			
MRATIBU WA KANDA			

BINAFSI

WATU WAPYA WALIOFIKIWA WATU WALIOFIKIWA KWENYE MAZINGIRA YA KUPANDA MAKANISA KULETA INJILI	
WAONGOFU WAPYA WAFUASI WA YESU	
WATU WAPYA WALIOBATIZWA WATU WALIOSHIRIKI KWENYE SAKRAMENTI YA UBATIZO	
VIONGOZI WAPYA KATIKA MAFUNZO WATU WANAOFUNDISHWA UONGOZI NA WAPANDAJI	

VIKUNDI VIDOGO | Kiwango cha chini wafuasi 2 wapya na kiongozi mmoja

VIKUNDI VIDOGO VIPYA VIKUNDI VILIVYOANZISHWA MWEZI HUU	
WASHIRIKI WAPYA KATIKA VIKUNDI VIDOGO WATU WAPYA WALIOSHIRIKI KATIKA VIKUNDI VIDOGO MWEZI HUU	
VIONGOZI WAPYA NA KIKUNDI VIONGOZI WAPYA NA KIKUNDI CHINI YA USIMAMIZI WA MPANDAJI	

MAOMBI UNAYOHITAJI

1. _____
2. _____
3. _____

SHUHUDA

KIPINDI CHA 1

KUHESABIWA HAKI KWA IMANI: MSINGI WA UHUSIANO WETU NA MUNGU (DK. 60)

Maelekezo ya Muwezeshaji: Kwa kutumia masomo hapo chini, elekeza kundi kuanza kujifunza Biblia katika mada ya haki. Waambie washiriki wajaze muhtasari ulioko hapa chini kwenye sehemu zao za kazi na kutoa maana ya haki kwa maneno yao wenyewe.

Utangulizi:

- Ni namna gani tunaweza kumfahamu Mungu kwa ukaribu, na kwa mahusiano yenye upendo?
- Je, kweli Mungu anatukubali?
- Je, kukubaliwa kwetu na Mungu kunatoka wapi?
- Ni namna gani tunaweza kuishi maisha yanayompendeza?
- Ni nini kinachotokea tunapotenda dhambi?

Mwanatheolojia wa Kikristo Millard Erickson aliandika,

Dhana fulani za fundisho la wokovu zinahusiana na suala la msimamo wa mtu na Mungu. Tabia ya mtu binafsi lazima ibadilike kutoka hali ya kuwa na hatia kwenda hali isiyokuwa na hatia. Hili ni suala la mtu kutangazwa kuwa mwenye haki mbele za Mungu, kuonekana ametekeleza matakwa yote ya Kimungu. Neno la kitheolojia hapa ni kuhesabiwa haki ... Kuhesabiwa haki ni tendo la Mungu kutoa tangazo, kama lile la hakimu kumwachilia mtuhumiwa ... Kuhesabiwa haki kuna uhusiano wa karibu na kuungana na Kristo.

KUJIFUNZA BIBLIA

- I. Kuhesabiwa haki SI
 - A. Kwa Matendo
 - B. Msamaha ambao kwa huo Mungu huzipotezea/hupuuza dhambi zetu
- II. Kuhesabiwa haki ni
 - A. Kuvikwa Haki ya Mungu: Warumi 3:21-24
 - B. Mbadilishano Mkuu: 2Wakorintho 5:21, Isaya 61:10, Warumi 4:3-5, 8:1, Waefeso 4:22-24
- III. Mambo muhimu ya Haki kwa Imani
 - A. Je, tunaweza kuijhesabia haki sisi wenyewe?
 - B. Je, tunaweza kuchukua utukufu kwa yale ambayo Mungu amefanya?

MATENDO – HUPUUZA – KUVIKWA HAKI – MBADILISHANO – SISI WENYEWE – MUNGU

Mfano:

Hebu mfikirie mtu ambaye amefanya dhambi kubwa na anasubiri adhabu ya kifo. Akiwa katika kusubiri, mmoja wa marafiki zake anaenda kwa jaji na kumuombea msamaha. Jaji anajibu, "nitamuachilia, ikiwa utanipa mwanaao afe kwa niaba yake". Rafiki anajibu, "huu ni ujinga. Nitawezaje kufanya hivi?" lakini jaji anasema, "Hii ndiyo njia pekee ninayoweza kumwachilia huru." Baada ya kuumia moyoni kwa muda mrefu, baba akaamua atamtoa mwanae kuwa dhabihu kwa ajili ya rafiki ... akijua hiyo ndiyo njia pekee. Kwa utii, mwanae akaenda kwa jaji na kukubali kufa kwa niaba ya rafiki wa babaye. Siku iliyofuata jaji akamtoa yule mtoto auae na akamuachilia huru yule rafiki. Mara baada ya haya, ikatokea baba alisikia mazungumzo kati ya mfungwa aliyeachiliwa huru na rafiki. Alipoulizwa, "Ilikuwaje ukaachiliwa huru kutoka kwenye adhabu ya kifo?" Yule aliyeachiliwa akajibu, "Nilipokuwa kifungoni nilijiweka katika hali ya usafi, nilikuwa na nidhamu, na nilifanya kile nilichoagizwa na walinzi. Kisha wakaniachilia kwa sababu ya tabia yangu njema."

Mjadala:

Unafikiriaje mwitikio wa huyu baba kwa kile rafiki alichokisema?

Inakuwaje huyu aliyeachiliwa afikiri kwamba tabia yake ilifanya chochote juu ya kuachiliwa kwake baada ya mwana kuyatoa maisha yake kwa ajili yake?

Je, ni lazima tumwamini Mungu kabisa, tena tumwamini Yeye pekee?

Ina maana gani tunapoelezea haki kwa imani kama "haki tunayopewa"?

Tunapotembea na Bwana kila siku, ni kwa nini ni ngumu sana kwetu sisi tunaonza katika neema kuendelea katika neema, kuiamini kazi ya Yesu Kristo iliyomalizikia msalabani?

Ni namna gani kuhesabiwa haki kwa njia ya imani kunaathiri uhusiano wako na Mungu na namna Mungu anavyohusiana na wewe?

Taswira:

Katika nafasi uliyopewa andika kwa maneno yako maana ya "kuhesabiwa haki kwa njia ya imani."

MPANGO KAZI KWA SOMO LA 5

Kabla ya kurudi katika Somo la 5, elekeza mtu mwingine au kundi dogo katika utangulizi huu wa kujifunza Biblia kwa uchimbuzi juu ya kuhesabiwa haki kwa imani, na kisha mwambie mtu au kundi waandike kwa maneno yao maana ya kuhesabiwa haki. Leta yale waliyoandika kwenye kipindi cha mafunzo yajayo.

Mapumziko (dakika 15)

KIPINDI CHA 2

KANUNI ZA KIBIBLIA ZA UONGOZI (DAKICA 60)

MAANA YA UONGOZI

Sema, “Chukua dakika moja kutoa maana ya neno ‘uongozi’ kwa maneno mafupi kwa kadiri iwezekanavyo kwenye nafasi iliyotolewa katika sehemu yako ya kazi.

Maana ya uongozi kwa maneno yangu:

Sema, “Mtafute mwenzako na mshirikishane maana ya uongozi kila mmoja wenu.”

Jadili yafuatayo katika kundi kubwa (lote)

- “Uongozi ni ushawishi, uwezo wa mtu mmoja kuweza kushawishi wengine” (Sanders, *Spiritual Leadership*, p.31).
- “Uongozi ni mchakato shurutishi ambapo mwanamke au mwanaume anakuwa na uwezo aliopewa na Mungu kuwashawishi watu wa Mungu kuelekea kusudi lake katika kundi hilo.” (Clinton, *Making of a Leader*, p.14; cf. p. 127).
- Linganisha maana yako ya uongozi na hiyo ya Sanders na Clinton.
- Neno moja lenye maana ya uongozi linaweza kuwa hivi uongozi ni “ushawishi.”
- Ni nini maana ya tafsiri ya uongozi kama “ushawishi?”
- Katika kanisa au huduma yako ni viongozi gani wana ushawishi kwa watu?

KANUNI ZA UONGOZI WA KIBLIBIA

Viongozi wa kidunia mara nyingi hufikiri kwamba “viongozi hawawezi kuwaamini watu walio chini yao wafanye kile walichotakiwa kufanya”, na kwamba, “kama utawaamini watu sana, watakudharau.” Viongozi wa kidunia wanaweza kuamini zaidi kwamba watu wanaweza kufanya kile unachowaelekeza pale tu utakapowapa motisha au kwa kuwatisha kwa adhabu. Kama matokeo ya fikra hizi, viongozi wa kidunia mara nyingi wanafikiri mamlaka ipo tu kwenye msingi ama wa nafasi waliyopo au kwenye nguvu ya hadhi yao.

VYANZO SABA VYA NGUVU

Hivi ni vyanzo saba nya nguvu. Vyote vinaweza kuwa vizuri au vibaya, inategemea namna vitakavyotumika. Unajihusianisha na vyanzo gani?

Muda/kukaa ofisini muda mrefu – hutegemea muda
 Nafasi – hutegemea cheo cha mtu
 Uwezo – hutegemea karama ya mtu
 Kicho – hutegemea kicho na thawabu/zawadi
 Heshima – hutegemea tabia na utashi
 Taarifa – hutegemea mawasiliano na ufahamu/ujuzi
 Mahusiano – hutegemea urafiki au mawasiliano na watu

Kutoka “Creativity and Innovation in Leadership,”
 Darasa la shahada ya uzamivu lililofundishwa na Dr. Larry Osborne

Mjadala:

Maelekezo ya Mwezeshaji: Masomo yafuatayo yanaelekeza mjadala wa kuonyesha tofauti kati ya uongozi wa Kidunia na wa Kikristo. Pata muda wa kusoma na kuandika kanuni za uongozi kutoka katika vifungu nya Maandiko vilivyotolewa. Wakati wa mjadala, waambie washiriki wajaze jedwali hapo chini.

Fikiria mahusiano yalivyokuwa kati ya mabwana na watumwa nyakati za Paulo, Waefeso 6:9 inatuambiaje kuhusu kuwadidimiza au kuwatia hofu watu walio chini ya uongozi wetu?

Je, ulishawahi kuumizwa na viongozi ambao walikuwa na tabia kama mawazo yanayoonekana hapo juu? Ilikuathiri vipi?

A. Mamlaka ya kuongoza hutoka kwa Mungu.

Maandiko yafuatayo yanatufundisha nini kuhusu mamlaka kama ilivyopangwa na Mungu?

MUNGU

- Serikali ya taifa ina mamlaka kisheria (Warumi 13:1-7, 1Petro 2:13-17)
- Familia (Waefeso 5:22-25, 6:1-4)
- Kanisa (Waebrania 13:17).
- Mfano wa Yesu (Yohana 8:28-29)
- Viongozi wa Kikristo huchaguliwa na Mungu (Yohana 15:16)

B. Utumishi wenyewe unyenyekevu lazima uwatofautishe viongozi wa Kikristo.

Je, maandiko haya yanatuambia kinyume cha utumishi ni nini? Jibu linalowezekana ni moja tu, ni kiburi.

- Bwana anachukia kiburi (Mithali 6:16-17)
- Mfano wa kuigwa wa Yesu (Wafilipi 2:1-8; Yohana 13:15)

C. Uongozi wa Kikristo unahitaji kukuzwa kwa kujifunza kwa umakini na kutendea kazi uliyojifunza

- Umakini katika kuendeleza uwezo wa kufundisha Neno la Mungu kwa usahihi (2Timotheo 2:15)
- Kuutawala mwili (Warumi 6:13, 1Korintho 6:20)
- Kustahimili majaribu (Yakobo 1:12)

Tofauti za Uongozi wa Kidunia na wa Kikristo

UONGOZI WA KIDUNIA	UONGOZI WA KIKRISTO
Kujiamini binafsi	Kujiamini kunakotokana na <u>Mungu</u>
Unawaelewa watu	Unamwelewa <u>Mungu</u> na <u>watu</u>
Hujiamulia wenyewe	Hutafuta mapenzi ya <u>Mungu</u>
Huhimizwa	Hupenda <u>kutumika</u>
Hutumia mbinu zake binafsi	Hutafuta na kufuata njia <u>za Mungu</u>
Hufurahia kuwaagiza wengine	Hufurahia kumtii <u>Mungu</u>
Huhamasika kwa matakwa yake binafsi	Huhamasika kwa <u>kumpenda</u> Mungu na watu
Hujitegemea wenyewe	Humtegemea <u>Mungu</u>

UTUMISHI WENYE UNYENYEKEVU - KUJIFUNZA – KUTENDEA KAZI – MUNGU – MUNGU – WATU – YA MUNGU – KUTUMIKA – ZA MUNGU – MUNGU – KUMPENDA – MUNGU -MBALIMBALI

Uliza: "Watu wanapozungumzia 'uongozi wa kawaida' je, mara nyingi wanasimamia hilo katika tabia za 'uongozi wa kidunia au uongozi wa Kikristo'?"

D. Biblia inaelezea mitindo mbalimbali ya uongozi.

Waefeso 4:11-12 inaelezea majukumu kadhaa ya uongozi yaliyokuwepo katika kanisa la Agano Jipy. Ijapokuwa yalikuwa yakinofautiana sana, kila moja lilifanya kazi ya "kuandaa watu wa Mungu kwa ajili ya kazi ya huduma" au, kwa maneno mengine, kuwaandaa watu wa Mungu kumtumikia na kutumikiana.

Kazi za Uongozi wa Agano Jipy

KARAMA	INAHUSU	KAZI
Mtume	Maono	Kuanzisha
Nabii	Dhambi	Kuhubiri
Mwinjilisti	Wokovu	Kufikia walio nje
Mchungaji	Kulea	Kufikia walio ndani
Mwalimu	Kweli	Kuelekeza

Mjadala katika kundi dogo:

Andika orodha ya shughuli katika "Mzunguko wa Kupanda Kanisa" katika Somo la 1 ubaoni. Shughuli ni maombi, Uinjilishaji, Kufuasa, Kukusanyika pamoja, Kuwakuza Viongozi, Kujizidisha, na Harakati. Kisha, katika makundi madogo (kama darasa ni kubwa), jadili Kazi za Uongozi wa Agano Jipy ambazo ni muhimu kwa kila hatua ya mzunguko.

*Mwendelezo wa Mjadala katika Kundi Kubwa:

E. Kazi ya awali ya uongozi wa kanisa ni kuandaa/ kukamilisha.

Je, Waefeso 4:11-12 inatuonyesha jukumu la msingi la kiongozi wa kanisa ni nini?

Viongozi Waelekezi na Wawezeshaji

KIONGOZI MWELEKEZI	KIONGOZI MWEZESHAJI
Analenga kazi: "anataka kazi ifanyike"	Analenga watu: "anawahusisha watu"
Mtendaji	Mgawa Majukumu
Lengo: "kufanya kazi ya huduma"	Lengo: "kuwaandaa wengine kutumika"
Mtendaji	Mwandaaji, mwezeshaji, mkufunzi

Zingatia: uongozi wote, elekezi na wezeshi unafaa katika huduma ya Kikristo. Kwa ujumla, uongozi elekezi unafaa pale unapowaongoza wengine walio na uzoefu mdogo katika jukumu wanalonakiwa kulitimiza na uongozi elekezi unafaa zaidi kwa watu ambao tayari wana kiwango kizuri cha ujuzi na uzoefu kwenye majukumu wanayoombwa kuyatimiza. Mtindo wa uongozi utatofautiana daima kulingana na kazi iliyopo na kiwango cha uzoefu wa wanaohusika. Hata hivyo, roho ya uongozi kwa mtindo wowote itambulike kwa sifa ya kumpenda Mungu na kuwapenda watu.

Uliza: Uongozi unaofaa zaidi kutumika kwa Wakristo ni 'Uongozi elekezi' au 'uongozi wezeshi?' Mwambie mtu mmoja atoe mfano wa hali ambayo inahitaji uongozi elekezi. Kisha mwambie mtu mwingine atoe mfano wa hali ambayo uongozi uwezeshaji unahitajika.

TASWIRA BINAFSI

Mwambie kila mshiriki arudi kwenye swali hapo chini na aandike kwa kifupi mwitikio. Kila mmoja akimaliza, shirikisha majibu machache kwa kila swali kwa ufupi kwenye kundi lote (kubwa).

- Watu huwa wanakuwaje viongozi katika utamaduni wako?
-
-

- Kwa nini ni muhimu kwamba viongozi wote kwanza lazima wawe wafuasi?
-
-

- Je, uelewa wako kwamba "mamlaka yako ya kuongoza yametoka kwa Mungu" unabadilishaje mtazamo katika uongozi wako?
-

- Nafasi gani zinachukuliwa pale mwamini mpya mwenye asili ya uongozi anapopewa uongozi kanisani?
-

-
-
- Ni zipi kati ya kazi tano za Uongozi katika Agano Jipya ambazo zimo ndani yako?
-
-

- Ni kwa njia zipi dhana hizi za kibiblia za uongozi zinatofautiana na kanuni za kidunia za uongozi?
-
-

VISA NA MIKASA

Maelekezo ya Mwezeshaji: Gawanya washiriki katika makundi madogo. Kila kundi lipatie kisa mkasa. Kwa kila kisa mkasa, waambie kila kundi liandike ni kanuni zipi za biblia zinazotumika au zisizotumika. Kwa kila hali, waambie kundi waamue namna watakayomshauri kiongozi kama wataitwa kwa tathmini. Kwa kufunga hii sehemu, waambie kila kundi dogo litoe taarifa yao kwa kundi kubwa na kuongoza mjadala mfupi kuhusiana na mwitikio wa kila kundi.

Angalizo: si muhimu kutumia visa mkasa vyote vilivyotolewa; chukua visa mkasa kadhaa vilivyotumika kwenye baadhi ya makundi ambavyo ni sahihi kwa ukubwa wa kundi lako.

1. Joseph amekuwa akiongoza mradi wa kupanda makanisa Kampala. Sarah na Ruth wamekuwa washirika katika kundi kwa miezi mitatu. Mara Sarah na Ruth wanaanza kujisikia ugumu mkubwa wa kutokuridhika na huduma. Wana mawazo mazuri sana ya uinjilisti lakini hawajisikii uhuru hata wa kuelezea mawazo yao. Kiongozi wao, Joseph, anaonekana hawezi kusikiliza maoni yao. Badala yake anawaambia nini cha kufanya na namna ya kukifanya. Matokeo yake, Sara na Ruth wanafikiria kuacha huduma na kuanza mambo yao mengine. **Ungeutathminije uongozi wa Joseph?**
2. Roberto anaongoza kundi la watu watatu katika kupanda makanisa huko Madrid. Roberto hutoa jumbe nzuri sana wakati wa kuabudu kila Jumapili asubuhi na huongoza vipindi vyta katikati ya wiki kwenye kundi dogo, ambalo limekua na kufika karibia washirika 20 waaminifu. Kila mmoja anafurahia uwezo wa Roberto wa kufundisha na kuhubiri Neno la Mungu, ni pamoja na uwezo wake wa kupanga shughuli. Hata hivyo, Roberto anaanza kujisikia kuchoka kutokana na mzigo wa kazi. Roberto anamwomba mwana kundi mwenzake Michael aanze kundi lingine dogo na

baadhi ya watu kutoka kwenye kundi la Roberto. Lakini, kunakuwa na mvuto mdogo, ambapo inamkatisha tamaa sana Michael. **Hebu tathimini namna Roberto atakavyoshughulikia kumhamishia majukumu Michael.**

3. Kanisa jipya huko kusini mwa sehemu ya Mkoa wa Loreto linakua kwa kasi kubwa. Wengi wanasema ukuaji huu ni kwa sababu ya uongozi bora unaotolewa na Alfredo na Anna. Wengi wa wahudhuriaji ni waamini wapya ambao hawafahamu kabisa hali ya nyuma ya kanisa. Kwa kuwa wamekua, Alfredo anaangalia ili kupata viongozi wapya watakaomsaidia katika kazi za kanisa. Lakini hakuna mtu mwingine tena anayeonekana ana viwango vya kuongoza. Anajisikia bahati kupata vijana watatu watakaoweza kufundishwa uongozi wa kanisa. Alfredo anapata ufadhili wa masomo kwa wawili wao kwenda kuhudhuria shule ya Biblia huko Lima. Wanaondoka kiangazi ili kwenda kuanza masomo kwa miaka 3. **Ungeitathmini vipi namna hii ya kuukuza uongozi?**
4. Akbar anaishi katika kijiji kidogo kaskazini mwa India ambacho hakina kanisa la kiinjili. Akbur sasa amefahamu kuwa waamini katika kijiji chake husafiri kutoka pande zote tofauti kuhudhuria kanisani – wengine kutoka umbali wa kilomita 30. Kwa uongozi wa Akbar, waamini wameanzisha kanisa jipya. Waamini wakusanyikapo pamoja, wana mwamko kuhusu kanisa la mahali pamoja na kila mmoja kwa utashi anashirikisha mawazo kuhusu kanisa litakavyopangiliwa kutokana na uzoefu wao wa makanisa waliyotoka. Lakini Akbar anaweka wazi kwamba yeye ndiye atakuwa mchungaji na watu wasahau kuhusu tamaduni na yale waliyokuwa wakifanya katika makanisa yao walikotoka, kwa sababu yeye ndiye mkuu kama mchungaji wa hili kanisa. **Unafikiri matokeo ya kile Akbar alichokiafiki yatakuwaje?**
5. Jacques amepanda makanisa matatu tofauti katika miji tofauti huko magharibi mwa Burkina Faso. Jacques kwa asili ni mpanda makanisa. Ni mtu mchapakazi na anayefikika kirahisi, mwenye karama ya Uinjilisti. Anapiga gitaa na kuimba na anaweza kuburudisha kusanyiko la watu kwa masaa mengi. Anapenda kuanzisha vitu na kisha kuendelea kwenye kitu kingine tena. Makanisa anayoanzisha yanaonekana kufanana naye tabia. Huwa wanapata nguvu sana mwanzoni lakini baada ya hapo wanadroofika kinapotokea kitu kingine. Jacques huchukulia kwamba hii ni tabia yake na kwa kweli hana namna anavyoweza kufanya abadilike. Anafahamu kuwa Mungu huwa anamtumia pamoja na hayo. **Ungeutathminije uongozi wa Jacques?**

6. John amekuwa akifanya bidii sana katika kupanda kanisa huko Sydney kwa miaka kadhaa. Kanisa linaendelea vizuri sana. Limekuwa hadi kufikia watu 200 miaka mitatu iliyopita. Mke na watoto wake wanne mara nyingine humaliza siku kadhaa bila kumuona kwa sababu huondoka asubuhi na mapema na kurudi usiku sana. John hapendi kuishi namna hii lakini watu wake ni wahitaji sana. Wengi ni wagonjwa na wanahitaji kutembelewa, na wasio na mahali pa kuishi wanahitaji kusikilizwa kila mara. John anafahamu kwamba akiacha kufanya hayo yote anayofanya, huduma itakuwa na shida, watu hawataokoka, na kanisa halitaendelea kukua tena. **Unafikiri John ni kiongozi mzuri? Kwa nini au kwa nini siyo?**

KIPINDI CHA 3

UINJILISTI NA UPANDAJI KANISA (DAKIKA 60)

Maelekezo ya Mwezeshaji: wagawanye watu kwa makundi ya 3 au 4. Waambie kila mtu ashirikishe uzoefu wake wa kufanya kazi na mchungaji anayemsaidia, kanisa na wengine wanaojumuishwa katika upandaji wao wa makanisa kuweka sawa maono, dhima, maadili ya msingi na mikakati yao. Nini kilitangazwa na kwa nini? Mabadiliko gani yalifanyika na kwa nini? Elekeza kundi kubwa litoe muhtasari wa mjadala wa kundi dogo.

TAARIFA YA MPANGO KAZI WA SOMO LA 4 (DAKIKA 30)

Kanuni za uinjilisti wa Kupanda Makanisa (dakika20)

Maelekezo ya Mwezeshaji: Kwa kutumia maelekezo hapo chini, elekeza kundi lijadili kanuni za uinjilisti kwa wapanda makanisa. Waambie washiriki wajaze sehemu zilizoachwa wazi katika sehemu zao za kazi.

A. Kutumia mahuiano ya kawaida kwa watu.

Ni mtandao gani wa mahusiano ambao Yesu aliutumia alipokuwa akiita wafuasi wake?
Yohana 1:40-41, 4:28-30, Luka 8:38-39

B. Waamini wapya hushuhudia papo hapo.

Kwa nini waamini wapya hutumika kama wainjilisti? Baadhi ya majibu ya kujadili sambamba na yako:

- Imani yao ni mpya
- Waamini wapya bado wana marafiki ambao si Wakristo ambao wanaweza kuona badiliko.

C. Nenda kwa Walinzi wa Lango.

Walinzi wa malango ni akina nani?

Watu wenye ushawishi au mamlaka juu ya wengine wanachukuliwa kama "walinzi wa malango" kwa sababu kuja kwao kwa Kristo kunaweza kufungua mlango kwa wengine kumkubali .

Kwa nini kufanya juhudi ya ziada kuwafikia? Jadili jibu hilo sambamba na wengine:

Wale wenye ushawishi mkuu wanaweza kusogea kwa Kristo taratibu, lakini mguso wao wa muda mrefu kwa injili unaweza kuwa mkubwa. Kutoka katika Maandiko haya, taja mifano ya majina ya "Walinzi wa malango" (Matendo 16:11-15, 17:1-9, 18:7-8).

D. Fikiria vizuizi nya kiutamaduni.

Namna gani unapanga kanisa liwafae watu unaoenda kuwafikia? (1 Waorintho 9:20-23)

E. Kuangalia kwa mtazamo wa kawaida.

Baadhi ya shughuli ambazo ni za kawaida kwa waaminio na wasioamini ni zippi?

MPANGO KAZI WA SOMO LA 5 (DAKIKA 10)

Kabla ya kurudi kwenye Somo la 5, tumia muundo wa Mpango Wangu Mkuu wa Kupanda Kanisa uliotolewa hapo chini kukusanya pamoja mpango mkuu ulioandikwa wa kanisa lako jipya. Washiriki wakutane na makanisa yanayowafadhili na wachungaji au walezi wao ili kuuhakiki mpango huu kabla ya Somo la 5.

MTAZAMO WA KAWAIDA

**MPANGO MKUU WA KUPANDA KANISA
WA**

(Jina la kundi la watu lililokusudiwa, wingi wa watu, au sehemu ya kijiografia)

IMEANDALIWA NA

(Jina lako)

IMEIDHINISHWA NA KUKUBALIWA NA

(Jina la mchungaji wa kanisa linalokufadhili au mlezi)

(Tarehe maandishi haya yalipothibitishwa na kanisa linalokufadhili na mchungaji)

I. Utafiti: Nini Mungu amenionyesha kuhusu watu niliokusudia, wingi wa watu, au eneo

A. Maelezo ya kawaida:

B. Nafasi ama milango iliyofunguka kwa ajili ya injili ambayo imegunduliwa:

C. Vikwazo vya injili na namna ya kuvishinda:

D. Mambo ya muhimu yatakayotoa taarifa ya juhud zangu za kupanda kanisa:

- a. _____
b. _____

- c. _____
d. _____
e. _____

II. Kauli ya Maono

Sehemu za Biblia zinazobeba Kauli ya Maono:

III. Kauli ya Dhima

Sehemu za Biblia zinazobeba Kauli ya Dhima:

IV. Kauli ya Maadili ya Msingi

Sehemu za Biblia zinazobeba Kauli ya Maadili ya Msingi:

V. Mpango Mkakati

A. Maombi:

- a. _____
b. _____
c. _____
d. _____

e. _____

B. Uinjilisti:

a. _____

b. _____

c. _____

d. _____

e. _____

C. Uanafunzi:

a. _____

b. _____

c. _____

d. _____

e. _____

D. Ushirika (kukusanyika pamoja):

a. _____

b. _____

c. _____

d. _____

e. _____

E. Kukuza Uongozi:

a. _____

b. _____

c. _____

d. _____

e. _____

F. Kuabudu:

a. _____

b. _____

c. _____

d. _____

e. _____

G. Ibada:

- a. _____
- b. _____
- c. _____
- d. _____
- e. _____

H. Kujizidisha (Dhima):

- a. _____
- b. _____
- c. _____
- d. _____
- e. _____

MCHUNGAJI

MPANDAJI

MWAKILISHI WA KANISA

Sahihi hii na tarehe vinathibitisha kanisa linalomfadhili na mchungaji au mlezi wamekubali na kubeba mpango huu wa kupanda kanisa.

Chakula cha mchana (dakika 60)

KIPINDI CHA 4

KUANZISHA KUNDI DOGO (DAKIKA 60)

MAFUNDISHO NA MIJADALA (DAKIKA 20)

Maelekezo ya Muwezeshaji: Tumia masomo yaliyopo hapo chini kuelekeza kundi lijadili namna ya kuanzisha vikundi vidogo. Waambie washiriki wajaze sehemu zilizo wazi kwenye sehemu zao za kazi wakati wa mjadala.

Elekeza kundi kuangalia kwa nini kila dondo ifuatayo ingekuwa ya muhimu katika kuanzisha kundi dogo:

1. Andaa Kundi Dogo Jipya
 - A. Anzisha Timu ya Waombaji (Waefeso 6:19, 1Wathesalonike 5:25)
 - B. Anzisha Timu ya Viongozi (Luka 10:1)
 - C. Tafiti Eneo Ulilokusudia
2. Fanya Mahusiano
 - A. Walengwa wa kusanyiko lako ni nani?
 - B. Ni kwa namna gani unaweza kuanzisha mahusiano nao?
3. Chagua Mahali/Eneo
 - A. Ni mahali gani panapofaa kwa kundi lako dogo kukutania?
4. Jiandae kwa Mkutano wa Kwanza
 - A. Ni matatizo gani yasiyo ya kawaida unayoweza kupata utakapokuwa “unaweka msingi” wa kupanda kanisa katika eneo ambalo halina mashahidi wa Kikristo?
 - B. Nini kinaweza kufanyika ili kushinda vikwazo hivi?
 - C. Ungemwambiaje mwamini ambaye ni sehemu ya kundi lako dogo na anahofia kuwakaribisha nyumbani wageni ambao hawafahamu?

KARATASI YA KAZI YA MPANGO WA KUNDI DOGO (DAKIKA 40)

Maelekezo ya Mwezeshaji: Waambie washiriki watumie Karatasi ya Kazi ya Mpango wa Kundi Dogo kutengeneza mpango wa kukutana. Ikiwezekana, wapatie nakala ya karatasi hii ya kazi ili kwamba washiriki watunze nakala safi kwenye vitabu vyao vya kazi. Washiriki wanaweza kutumia hii karatasi safi ya kazi kutoa nakala zaidi za mpango wa mikutano ya

ANDAA - TIMU YA WAOMBABI - TIMU YA VIONGOZI - TAFITI - MAHUSIANO - KUSANYIKO - MAHUSIANO - MAHALI/ENEO - PANAPOFAA - JIANDAE

kundi dogo.

1. Ni sehemu gani ya mpango ilikuwa rahisi kwako? Kwa nini?
2. Ni sehemu gani ilikuwa ngumu zaidi? Kwa nini?
3. Ungefanya nini kama usingepata mtu mwenye uwezo wa kuimba na ambaye angeweza kuongoza kundi kuimba?
4. Ni sehemu gani za mukutano wa kundi dogo ungetarajia ziende vizuri? Elezea.
5. Ni sehemu gani ulitarajia zingeenda vibaya? Elezea.

Karatasi ya Kazi ya Mpango wa Kundi Dogo

Tarehe na siku ya kuonana: _____	
Mahali na mwenyeji: _____	
USHIRIKA	
Viburudisho: _____	
Shughuli, michezo: _____	
KUABUDU	
Kiongozi wa Uimbaji: _____	
MAOMBI	
Maombi: _____	
MJADALA WA BIBLIA	
Kiongozi wa mjadala: _____	
Kifungu cha maandiko: _____	
MATARAJIO YA HUDUMA	
Wakati wa kushirikishana: _____	
Shughuli: _____	

Maelekezo ya Mwezeshaji: katika dakika 10 za mwisho za kipindi, tumia maswali yafuatayo kutoa muhtasari wa shughuli ya mpango binafsi.

MAMBO YA KUFIKIRIA:

- Kiongozi wako mkufunzi ni nani?
- Ni nani anayetoa nidhamu kwa kila mshiriki wa kundi lako?
(Unamnidhamisha nani?)
- Unafanya nini kumsaidia kiongozi wako mkufunzi kukuza ujuzi wake wa uongozi?
Ni namna gani unamgawia/ unampatia huduma? Ni kwa namna gani unakuwa kielelezo cha huduma kwake?
- Je, unamuombea kila mshirika katika kundi lako dogo?

KIPINDI CHA 5

UINJILISTI NA KUFIKIA MAHITAJI YA JAMII (DAKICA 60)

Maelekezo ya Mwezeshaji: Toa utangulizi wa aina tatu za mahusiano kati ya huduma na uinjilisti. Waambie washiriki wajaze kwenye sehemu zilizo wazi katika vitabu vyao vya kazi. Kisha gawanya katika makundi matatu. Bandika karatasi tatu kwenye kuta tatu tofauti ndani ya chumba. Katika karatasi ya 1 andika "Matokeo" karatasi ya 2 "Daraja" na karatasi ya tatu "Ambatana". Mpe kazi mmoja katika kila kundi. Liambie kundi liende kwenye karatasi na kupendekeza idadi nyingi ya shughuli za huduma na uinjilisti wanazofikiri kwa mahusiano waliyopewa. Baada ya dakika 10, yaambie makundi yazungukie kwenye karatasi inayofuata na kurudia zoezi wakiongezea kazi kwenye kundi lililopita. Waendelee kuzunguka kila dakika 10 mpaka kila kundi lichangie kwa kila karatasi 3. Tumia dakika 10 za muda uliobaki kutoa muhtasari wa shughuli kwenye kundi kubwa. Hitimisha kwa kuwaruhusu washiriki kwa muda uliobaki warudi kwenye karatasi na kuandika kwenye nafasi zilizotolewa kwenye vitabu vyao mawazo wanayoamini yanaweza kuwa msaada kwao katika sehemu ya kupanda kanisa.

AINA TATU ZA MAHUSIANO KATI YA HUDUMA NA UINJILISTI

1. Huduma kama MATOKEO ya uinjilisti: Mawasiliano yetu na Kristo hutufanya kuwa wasikivu kwa mahitaji ya wengine na kuwa tayari kuyafikia.
-
-
-

2. Huduma kama DARAJA la uinjilisti: huduma kwa wengine kama hatua ya awali ambayo hatimaye huwafanya kuwa tayari kuisikia injili.
-
-
-

3. Huduma INAYOAMBATANA na uinjilisti: tunanena habari za Yesu na wakati huo huo tukiwahudumia wengine.
-
-
-

Mapumziko (dakika 15)

KIPINDI CHA 6

KUTAFSIRI NENO LA MUNGU: KWA KUTUMIA MAFUNZO YA BIBLIA KWA NJIA YA UCHIMBUZI (DK. 60)

MARUDIO (DAKICA 20)

Waambie washiriki: wakumbuke hatua tatu za maelekezo ya mchakato wa kujifunza Biblia kwa kutumia sehemu zilizo wazi zilizotolewa hapo chini (kutoka Somo la 1).

- A. Uchunguzi – linasemaje?
- B. Tafsiri – lina maana gani?
- C. Matumizi – ninatakiwa nifanye nini?

Waambie washiriki: wakumbuke hatua za msingi za kipindi cha kuchunguza maelekezo ya kujifunza Biblia kwa kutumia nafasi zilizo wazi zilizotolewa hapo chini (kutoka Somo la 2)

- A. Jiandae kwa uchunguzi.
- B. Chukua muda wa kutosha.
- C. Angalia mazingira (au hali)
- D. Chunguza muundo.
- E. Uliza maswali ya kipelelezi.

MAWASILISHO (DAKICA 20)

Maelekezo ya Mwezeshaji: Tumia mfumo wa kufundisha, waambie washiriki wakamilishe nafasi zilizo wazi zifuatazo kuhusiana na hatua za utafsiri wa maelekezo ya kujifunza Biblia.

1. **Tafsiri - Hatua ya Pili ya Mbinu ya Uchimbuzi**
2. **Mchakato wa Uchimbuzi**
 - I. Rejea kweli za uchunguzi wa msingi wa kifungu
 - II. Tafuta dondoo kuu ya mwandishi.
 - III. Tafuta mtiririko wa mawazo kwenye kifungu
3. **Sheria za Msingi za Kutafsiri**
 - I. Kanuni za Kawaida za Kutafsiri Biblia
 - a. Biblia ni Neno la Mungu lenye Mamlaka

LINASEMAJE - MAANA - NIFANYE - JIANDAE - MUDA - MAZINGIRA - MUUNDO - KIPELELEZI - TAFSIRI - UCHIMBUZI - KWELI - DONDOD KUU - MTIRIRIKO WA MAWAZO - SHERIA - KANUNI - LENYE MAMLAKA

- b. Biblia ndio mtafsiri mwenyewe aliye bora, ikiakisi tabia ya Mungu.
 - c. Imani iokoayo na Roho Mtakatifu ni muhimu ili kuyaelewa Maandiko.
 - d. Unatafsiri historia, matendo, tabia, uzoefu binafsi, n.k. katika nuru ya Maandiko.
 - e. Kusudi la awali la Biblia siyo kutuongezea maarifa bali ni kuyabadilisha maisha yetu.
 - f. Kila Mkristo ana haki, wajibu, na upendeleo wa kuchunguza na kutafsiri Neno la Mungu kwa msaada wa Roho Mtakatifu.
4. Kanuni za Kutafsiri Biblia Kisarufi, Kihistoria, na Kitheolojia
- a. Unatafsiri maneno kulingana na maana zake kwenye mazingira ya kihistoria na kiutamaduni ya mwandishi. Kila mara fikiri kuhusu jinsi ambavyo wasikiaji wa awali wangelewa na kujibu ujumbe.
 - b. Ni muhimu kuelewa sarufi ya kifungu kabla hujajaribu kuelewa ukweli unaofundishwa kitheolojia.
 - c. Lugha ya kimafumbo kwa kawaida ina dondo kuu moja. Usijaribu kusoma vitu vingi kwenye kifungu kilichotumia fumbo/mfano au lugha iliyojificha kwa mawazo.
 - d. Usiwe muelewa zaidi wa somo kuliko Maandiko yanavyoolewaka. Usiongeze mawazo yako au tamaduni za kanisa lako kwenye kile Biblia inachosema, maana wewe au wengine mnaweza kuja kuamini hayo mawazo ni Maandiko halisi.
5. Makosa ya kawaida ya Kitafsiri ya Kuepuka
- a. Kurukia: kuruka kutoka kwenye kifungu kimoja kwenda kwenye wazo tofauti au mafundisho mnayotaka kujadili.
 - b. Mfano: kudharau maana ilijo wazi ya Andiko na kujaribu kutafuta maana iliyojificha.
 - c. Kudharau Ufunuo Endelevu: kusahau asili endelevu ya Andiko.

MTAFSIRI - ROHO MTAKATIFU - MAANDIKO - KUYABADILISHA MAISHA YETU - HAKI - WAJIBU - UPENDELEO - ROHO MTAKATIFU - KISARUFI - KIHISTORIA - KITHIOLOJIA - KIHISTORIA - KIUTAMADUNI - AWALI - SARUFI - MOJA - USIONGEZE - MAKOSA - KURUKIA - MFANO - KUDHARAU UFUNUO ENDELEVU

MATUMIZI YA KUNDI DOGO (DAKIKA 30)

Maelekezo ya Mwezeshaji: Wagawanye katika makundi madogo na mkamilishe shughuli ya zoezi la kutafsiri hapo chini. Waambie watu wajitolee kuhudumu kama wawezeshaji wa somo kwa kila kundi. Kazi ya mwezeshaji ni kuendeleza kundi kujifunza. Toa muhtasari wa uzoefu kwa kadiri muda utakavyoruhusu.

Maelekezo ya Kundı: Rejeeni nyuma kwenye uchunguzi wa Yeremia 1 uliokamilika katika Somo la 2. Pitia mchakato wa kutafsiri kwa kadiri muda utakavyoruhusu. Fuata mfumo unaoonyeshwa hapa chini.

1. Tafuta jibu la uchunguzi wa kifungu
2. Thibitisha wazo kuu.
3. Elezea mtiririko wa mawazo.
4. Rejea katika baadhi ya maswali ya “muhimu”.

Utakapokuwa unashughulikia sentensi hizo hapo juu, inaweza kukusaidia kufikiri kuhusu maswali yanayohusiana na maana ya andiko. Inawezekana ukafikiria maswali mengine mazuri au hata bora zaidi. Haya yametolewa kukuanzishia mchakato.

Mstari wa 5

Inamaanisha nini kwamba Bwana “alimfahamu” Yeremia? “Kutengwa” kuna maana gani?

Nini maana ya sentensi “...kabla hujazaliwa nalikutenga...”?

Mstari wa 6

Kwa nini Yeremia (inawezekana) alijiona “mtoto”?

Kwa nini unafikiri Yeremia aliitikia kwa jinsi alivyoitikia?

Mstari wa 7

Unaelezaje wito wa Mungu kwa hiki ulichoona katika mstari huu? Nini jibu lako la swalii lililopita linalosema kuhusu Mungu na tabia Yake?

Mstari wa 8

Maneno ya Bwana yanasmaje kuhusu mwitikio wa watu katika huduma inayokuja ya Yeremia?

Ni msukumo gani uliopo kwa Yeremia kuwakabili maadui zake?

Mstari wa 9

Ni namna gani Mungu “aliweka” maneno yake kwa Yeremia?

Mstari wa 10

Unafikiri misemo “kung’oa, kuharibu na kuangamiza, kujenga na kupanda” ina maana gani?

Unafikiri kuna nini juu ya tabia ya Yeremia ambayo itamruhusu kuufuata mpango wa Mungu?

Mstari wa 12

Ni kanuni gani umeipata katika mstari huu kuhusu Mungu kuhusika kwenye huduma ya wote wamwitao?

Mstari wa 16

Mstari huu unaonyesha nini kuhusu tabia ya Mungu, hata linapokuja suala la kuhukumu watu Wake mwenyewe?

Je, Mungu alitenda haki kile alichopanga kuwafanya watu wake? Kwa nini?

Mstari wa 17

Ni nini kinachoweza kuwa sehemu ya “kujiweka tayari” kwa Yeremia?

Kwa nini unafikiri Bwana alirudia tena kile alichokuwa ameshasema kabla (mst wa 8)?

Mstari wa 18

Nini maana na umuhimu wa misemo “mji wenye boma, nguzo ya chuma na kuta za shaba”?

Kwa nini watu wa mstari wa 18 walimpinga sana Yeremia na ujumbe wake?

Je, Mungu huwaimarishaje watu wake na kuwaandaa kusimama kwa ajili yake leo?

Mstari wa 19

Mstari huu unaonyesha nini kuhusu tabia ya Mungu na uwajibikaji wake kwa wote wamwitao?

KUFUNGA

NI NINI KINACHOFUATA?

Kabla hujafika kwenye somo linalofuata, tunashauri ufanye yafuatayo:

- Fanya mahusiano mapya 10.
- Fikisha injili kwa watu 5.
- Anzisha kundi jipya dogo.

- Tathmini kazi mbili za Mipango Kazi ya Somo la 5: (1) Ongoza mafunzo ya Biblia juu ya kuhesabiwa haki (angalia Kipindi cha 1 cha mwongozo huu) na, (2) Kamilisha Mpango Mkuu wa Kupanda Kanisa (angalia Kipindi cha 3 cha mwongozo huu).
- Waambie washiriki wakumbuke Kanuni 5 za Uinjilisti kwa Wapanda Makanisa (angalia Kipindi cha 3).
- Waambie washiriki wakumbuke aina 3 za mahusiano kati ya Huduma na Uinjilisti (angalia Kipindi cha 5).
- Waambie washiriki washirikishe kitu ambacho wamejifunza katika mafunzo ambacho kimewaamsha upya, kuwatia moyo, au kuwapa motisha katika kazi yao kama wapanda makanisa.
- Waambie washiriki watengeneze malengo ya kupanda kanisa kwa mwezi huu (angalia jedwali hapo chini).
- Imbeni wimbo wa kuabudu pamoja na kufunga kwa maombi ya kuwabariki wapanda makanisa hawa.

MALENGO YA KUPANDA KANISA KWA MWEZI HUU	
WATU BINAFSI	
Mahusiano mapya	Idadi tafadhali
Waamini wapya	Idadi tafadhali
Watu wapya waliobatizwa	Idadi tafadhali
Viongozi wapya katika mafunzo	Idadi tafadhali
MAKUNDI MADOGO	
Makundi mapya madogo	Idadi tafadhali
Washiriki wapya katika makundi madogo	Idadi tafadhali
Viongozi wapya na makundi madogo	Idadi tafadhali